



Dua hairejeshwi (inayoombwa) baina ya adhana na kukimiwa swala

Imepokelewa kutoka kwa Anas bin Maliki -radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-
Amesema: Amesema Mtume -rehema na amani ziwe juu yake: "Dua hairejeshwi
(inayoombwa) baina ya adhana na kukimiwa swala".

[Sahih]

Amebainisha Mtume rehema na amani ziwe juu yake fadhila za dua baina ya adhana na ikama, nakuwa dua hiyo hairejeshwi na inanafasi kubwa ya kujibiwa, basi muombeni Mwenyezi Mungu ndani ya wakati huu.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/5479>

النجاة الخيرية
ALNAJAT CHARITY

